

**HOTUBA YA NAIBU KATIBU MKUU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI
YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, BW. XAVIER DAUDI
KWENYE UFUNGAJI WA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI
MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC – JIJINI ARUSHA,**

FEBRUARI 8, 2024

*Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb); Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti
ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Mhe. Emmanuela Mtatifikolo Kaganda, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa
wa Arusha,*

*Dkt. Jasmine Tiisekwa; Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

*Mha. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali
Mtandao (e-GA),*

*Bw. Yusuf Hamad; Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya
Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi
mbalimbali,***

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya

Serikali Mtando,

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima, afya njema na kutuwezesha kuwa hapa leo.

Kwa heshma kubwa, nakushukuru sana **Mhe. Naibu Waziri**, kwa kukubali na kuitikia wito wetu wa kushiriki nasi hapa leo. Natambua kuwa Ofisi yako ina majukumu mengine muhimu ya kitaifa, lakini umeweza kutenga muda ili ushiriki nasi leo katika hafla hii ya kuhitimisha kikao kazi hiki muhimu cha Serikali Mtando. Hii, inadhihirisha dhamira ya kweli ya ofisi yako na wewe binafsi katika kusimamia maendeleo ya Serikali Mtando. Tunakushukuru sana na nakukaribisha tena kwa mara nyingine.

Aidha naushukuru uongozi wa Mkoa wa Arusha kwa amani na utulivu wa himaya hii kwa kipindi chote cha siku tatu (3) za Kikao Kazi hiki. Hakika tumekuwa salama muda wote wa kikao, hivyo tunawashukuru sana kwa ulinzi na ukarimu mliotupatia.

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru pia waandaaji wa Kikao Kazi hiki, yaani Mamlaka ya Serikali Mtando (e-GA), kwa kweli kimekuwa ni kikao cha mfano na mambo mengi hapa yamefanyika kidijitali, hongereni sana. Kwa kweli, e-GA mmeonesha mfano wa utekelezaji wa azma ya

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya ujenzi wa Serikali ya Kidijitali.

Niwashukuru pia viongozi na watumishi wa Serikali, Mashirika na Taasisi binafsi, ambao mmejumuika nasi katika kikao kazi hiki kwa muda wote huu. Ni wazi kuwa uwepo wenu hapa mmeweza kutoa maoni na michango mbalimbali itakayosaidia katika jitihada za kukuza na kuimarisha Serikali Mtandao. Niwapongeze na kuwasahi kudumisha ushirikiano huu ambao ni tunu kwa maendeleo ya nchi yetu kwa vizazi vyote.

Vile vile, Ninapenda kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Mkutano huu hususan wadhamini wote mlajitokeza kuchangia kikao kazi hiki. Michango yenu ya hali na mali hakika imewezesha tukio hili kufana na kuwa la aina yake.

Ninawaomba kwa umoja wenu muendelee kuona umuhimu wa kusaidia tena jitihada kama hizi kwa vipindi vijavyo.

Nipende pia kuwashukuru washiriki wote walioshiriki Kikao hiki niseme tu kuwa nimefarijika kwa namna mlivyoshiriki kikamilifu katika majadiliano, pamoja na kutoa maoni na ushauri katika masuala mbalimbali yaliyowasilishwa yenye lengo la kuimarisha na kukuza utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

Mhe. Naibu Waziri,

Kikao Kazi hiki cha Nne (4) cha Serikali Mtandao, kililenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao kutoka katika Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma ili kujadiliana kwa pamoja kuhusu hali ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi mbalimbali za umma, ikiwemo changamoto zilizopo na mbinu za kukabiliana nazo.

Mhe. Naibu Waziri,

Tangu vikao hivi vilipoanzishwa, Tumeshuhudia manufaa makubwa katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, zimekuwa zikiimarika na kukua siku hadi siku kupitia mawazo na michango mbalimbali yanayotolewa na washiriki katika vikao hivi.

Kwa pamoja tumeazimia kuwa yale yote yaliyojadiliwa humu, tutayafanya kazi kwenye ngazi mbalimbali za utendaji chini ya usimamizi wa e-GA, lengo likiwa ni kuboresha utendaji kazi wa shughuli mbalimbali za Serikali na utoaji wa huduma kwa umma.

Baada ya kusema haya machache naomba basi kumkaribisha Mgeni Rasmi **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete; Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** ili aongee nanyi na kutufungia kikao kazi hiki.

Karibu Mhe. Naibu Waziri.

ASANTENI